Ruzuku za shughuli za burudani zilizoandaliwa

Mamlaka ya Manispaa ya Nordre Follo inataka watoto na vijana zaidi kushiriki katika shughuli za burudani zinazoandaliwa mara kwa mara. Kwa madhumuni haya, Mamlaka ya Manispaa imeanzisha mpango wa ruzuku ambao vilabu, vyama na wafanyakazi wa manispaa wanaweza kuomba.

Unaweza kupata msaada gani?

Unaweza kupata msaada wa gharama zinazohusiana na shughuli za kawaida zilizopangwa. Mifano ni pamoja na ada za uanachama, leseni, ada za mshiriki / shughuli, na gharama zingine zinazohusiana na shughuli. Mamlaka ya Manispaa haitoi msaada wa shughuli binafsi na ada ya uanachama kwenye ukumbi wa mazoezi.

Nani anaweza kupata msaada?

Watoto na vijana wenye umri kati ya miaka 6-18 waliosajiliwa kama wakazi katika manispaa ya Nordre Follo ambao hawawezi kumudu kushiriki katika shughuli ya burudani iliyoandaliwa wanaweza kupata msaada. Tunakagua kila ombi wenyewe na tunaweza kutoa sehemu au kiasi chote unachoomba.

Nani anaweza kuomba (kwa niaba ya mtoto au kijana)?

Familia na watu binafsi hawawezi kuomba ruzuku wenyewe; badala yake wanapaswa kuwasiliana na mfanyakazi wa manispaa au mtu / shirika linalotoa shughuli hiyo. Kisha mtu huyu atatathmini ikiwa mtoto anatimiza vigezo vya kupokea ruzuku.

Ili kupokea msaada wa shughuli, mtu anayehusika na shughuli hiyo sharti awe amesajiliwa katika Sajili ya Mashirika Yasiyo ya Biashara. Pia tunatoa msaada kwa shughuli za manispaa kama vile shule za utamaduni na vilabu vya vijana.

Ombi sharti liwe na jina la mtoto / kijana, tarehe yake ya kuzaliwa, na idhini kutoka kwa mzazi au mlezi anayetambulika kisheria wa watoto wenye umri wa chini ya miaka 15.

Kutuma Ombi

Mratibu wa shughuli au mfanyakazi wa manispaa hujaza fomu ya ombi na kutuma ombi kwa Mamlaka ya Manispaa kwa njia ya kielektroniki. Sharti utume ombi tofauti la kila mtoto. Maombi hayapaswi kujumuisha gharama za safari au shughuli nyingi. Hakuna tarehe ya mwisho ya kutuma maombi.

Fomu ya ombi

Nani huchakata maombi?

Idara ya Afya ya Umma, Michezo na Shughuli za Nje hupokea na kutathmini maombi kulingana na miongozo ya mpango wa ruzuku. Tunachakata data zote za kibinafsi kulingana na miongozo husika.

Kupokea jibu la ombi

Kwa kawaida wanaotuma ombi watapokea majibu ndani ya siku kumi. Mamlaka ya Manispaa italipa kiasi cha ruzuku kwa mtu au shirika linalotoa shughuli hiyo.

Ikiwa una maswali au unahitaji usaidizi wa kutuma ombi

Wasiliana na mratibu wa afya ya umma Heidi Berentsen
Simu: (+47) 90 10 27 08